**[R1889]**

## KWA UZURI NA UTARATIBU

---

"Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na utaratibu."—***1 Wakorintho 14:40***.

HIVI KARIBUNI,kwa njia yoyote miongoni mwa kusanyiko la watakatifu, mawazo yetu yamekuwa katika mada hii ya utaratibu katika Kanisa.Vile idadi ya wale wanaotengana na "Babeli" kwa mundu wa ukweli wanaongezeka,na katika kundi dogo au kubwa linalokusanyika kama ilivyokusudiwa na Bwana ( ***Waebrania 10:25***), twaona ugumu mpya na hatari mpya ikienea,hasa kwa shughuli za adui wetu aliye makini sana.Hii imetufanya tuwe makini tena kwa mada yetu kulingana na Maandiko.

Mitume walikuwa na mambo mengi ya kuwaambia Kanisa kuhusu utaratibu katika makusanyiko ya watakatifu;na leo hii tumepuuzia kiasi ushauri huu wa hekima,tukidhania kwamba haina umuhimu sana,kwa sababu Kanisa liko karibu kumaliza kazi yake na mavuno ni wakati wa kutengana.Lakini ni vizuri kuangalia kwa makini kwamba " mambo hayo yaliandikwa kutufundisha sisi." Japo wakati umekuwa mfupi na kukaa kwetu duniani umekaribia kuisha,masuala katika vita na uwezo wa nguvu za giza vinazidi kuwa muhimu sana na mashindano ya kila mmoja yanakuwa kali na yakupambanua.

"Wakati ni ukweli kwamba mavuno ni wakati wa kutengana,pia tujue kwamba ni wakati wa kukusanya.Je,mkulima anaweza kuridhika akipurura nafaka na kuacha zikiwa zimetapakaa ardhini? La hasha,yuajua ya kwamba asiposanya nafaka na kuzihifadhi basi kazi yake itakuwa bure:itaoza juu ya ardhi,ama ndege watakuja na kuzila.Basi Bwana ni mume mwenye hekima,na yuatambua kwamba wale wanaotengana na wanaokusanyika ni sehemu ya kazi ya mavuno,na anasema, "Tokeni kwake,enyi watu wangu [ mjitenge na Babeli];" na pia , "Nikusanyieni wachao Mungu wangu waliofanya agano nami kwa dhabihu."

Sisi basi,tuliotengana kutoka Babeli hatupaswi kusimama peke yetu na kutengana na wenzetu,lakini tunapaswa kukusanyika pamoja katika ushirika wa Ukristo na kukula pamoja kwenye meza ya Bwana-yaani meza ya mavuno,ambayo imetengenezwa kwa njia ya kifahari. " Kwa kuwa po pote ulipo mzoga (chakula),ndipo watakapokusanyika tai [ wale walio na njaa na wanaoona mbali,ambao wanaona chakula kutoka mbali] ." (***Mathayo 24:28***).Twapaswa kukusanya pamoja na kuimarisha upendo na ushirikiano sana " kadri tunavyoona siku ikikaribia." Na kwa hivyo ni suala muhimu kwamba tuwe makini kuangalia yale ambayo Maandiko yanasema kuwa ni ya muhimu katika makusanyiko ya watakatifu.

## UTARATIBU KATIKA KANISA LA AWALI

---

Katika Kanisa la awali,vyombo vya uchapishaji havikuwa vikifanya kazi kwa huduma ya kusambaza ukweli,na hata nakala za muswada wa Neno la Mungu haukuwa kwa mikono ya

watu;na hata watu wengi hawakuwa na uwezo wa kusoma.Agano Jipya pia,lilikuwa kwa harakati ya kuundwa.Wakati huo Mitume walibadilisha barua miongoni mwa makusanyiko na kunakili ili kuangaliwa na kutoa maagizo.

Kukosa kwao kwa vitu tulivyo navyo,hata hivyo, kulikuwa wa msaada kwao na ulifanywa na Mkuu wa Kanisa katika karama-ya kuongea kwa lugha,kutafsiri lugha,unabii,n.k..,vitu ambavyo vimepitwa na wakati,kama vile Paulo alivyotangaza kwamba vitapita (***1 Wakorintho 13:8***),na kuanzishwa na baraka nyingi za nyakati hizi-Neno la Mungu lililoimara na limekamilika katika mikono ya watu,ambao elimu imewafikia wote;pamoja na vifaa vinavyosaidia kuelewa kama Kitabu cha Alphabeti cha Biblia,Kamusi za Biblia,n.k.,

Ili kwamba mikutano ya Kanisa uwe wa faida katika siku za awali kulikuwako na mpangilio wa masuala yao uliofanywa na mitume,na kufuatwa na makusanyiko ya watakatifu.Wale waliokuwa na karama ya ndimi,ama kufasiri ndimi,au unabii,hawakuwa wakiongea kwa pamoja;wanawake ambao hawakusoma na hawana elimu wa siku hizo (hasa katika Kanisa lililoko Korintho) hawakuruhusiwa kuingilia kati na kuwachanganya mikutano,n.k,n.k.Na huduma nzima ulikuwa na hadhi,unyofu na utulivu;japo na uwepesi,kila kitu kilikuwa kikifanywa kwa njia ya utaratibu,wakati baada ya wakati,kulingana na uwezo wao tofauti,wakichukua nafasi ya kusaidia kujenga mwili wa Kristo.Wengine walikuwa na uwezo wa kushauri Kanisa katika mafundisho ya ukweli;wengine walikuwa na karama ya kuongea kwa ndimi au kutafsiri ndimi;wengine walikuwa na uwezo wa kuhimiza na kutia moyo;na wote walikuwa na uwezo wa kuunga mioyo yao katika dua na kuinua sauti katika sifa,katika zaburi na tenzi za Roho. ( ***1 Wakorintho.14:15;Waefeso 5:19;Wakolosai 3:16***.) Kwa hiyo waliweza kuzoeana na walikuwa wanasaidiana,na kwa pamoja ili wazidi katika ukuaji na kuendelea katika Ukristo,njia yao ya kujenga maadili yaliyotolewa na Bwana,na kwa njia yao ya utaratibu kupitia kwa ushauri wa mitume.

Wakati huu utaratibu ulionyeshwa katika mikutano yao,na ulitekelezwa na Kanisa,kulikuwa pia na utaratibu katika viongozi na wajibu mbalimbali ya Kanisa.Kwa hiyo,kwa mfano,Paulo na Barnaba,wakati walikusanya makutano ya waumini katika Listra,Ikonio na Antioko, " wakachagua wazee katika Kanisa;" na wakawaweka katika mikono ya Bwana wakatoka. ( ***Matendo 14:21-23***.)Paulo pia alishauri Tito aende kwa kila mji akiwachagua wazee,ambao wajibu wao ilikuwa ni kuangalia Kundi la Bwana lililoko karibu,kuwalisha na ukweli,kuwalinda dhidi ya mbwa mwitu waliovaa kama kondoo,na kwa jumla,kuwa kama wawakilishi wao. (***Tito 1:5;Matendo 14:23;20:17,28;1 Petro 5:1,2;Matendo 15:6,23-28***).Kufuzu kwa wazee hao pia kulielezwa na Mitume-***1 Timotheo 3:1-13;Tito 1:5-11***.

**UTARATIBU UNAOTAKIKANA LEO HII**

Ikiwa utaratibu huu ulikuwa wa muhimu kwa ufanisi wa Kanisa la awali,kwa sababu kilicho muhimu kiliwekwa pamoja na kufanywa na watu wote,ili kwamba hatukuwa na mwanya wa

kutawala kwa njia yo yote,basi kuna swali la kuulizia kama ikiwa umuhimu huo bado upo miongoni mwa makundi ya watakatifu leo hii.

Tunaamini kwamba umuhimu huo wa mpangilio na uchaguzi wa wazee bado upo leo hii,na kwa sababu muhimu ambazo zilifanya ziwe kwa wakati huo zipo,ambazo ni zifuatazo:—

(1) Kwa sababu katika Kanisa,kama vile familia,kuna viwango tofauti ya usitawisho wa kiroho.Wengine ni wachanga,na wanahitaji maziwa kamili ya Neno,wakati wengine wanahitaji nyama ngumu;na inahitajika basi kwamba mtu “ aliye na uwezo wa kufundisha” awe katika hali ya kufanya hivyo.Kunayo pia majaribu,mateso,magumu na hatari ambayo hakuna aliye tayari kukumbana nazo.Kwa hivyo kunahitajika waangalizi wenye hekima na tahadhari,watu walio na uzoefu na uwezo,ambao wana hamu katika kuangalia maslahi ya kiroho kwa wote,na anaweza kuwaagiza katika ukweli.

(2) Kwa sababu miongoni mwa Kanisa la awali kulikuwako na mbwa mwitu waliojivaa ngozi ya kondoo ambao “walileta uzushi wa kupoteza,” ambao wazee waliochaguliwa wanapaswa kuwalinda dhidi yao,ambao pia wanapaswa kulishika kwa kuwaongoza kwa maarifa ya ukweli.Wakati huo pia,Mtume Paulo alitangulia kutuonya, “tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotofu,wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.” Na wazee waaminifu watakuwa na wepesi wa kutambua na kujaribu kuwaonya na kuwatetea makundi dhidi ya ushawishi wote wa namna hiyo.-***Matendo 20:28-30;Tito 1:10-11;2 Petro 2:1-3***.

(3) Kwa sababu ikiwa mipangilio na mateuzi hayangefanywa kwa njia inayotakikana na Mitume,mtu angechukua uongozi na kushikilia kwa muda usiojulikana;na kwa njia nyingine mkutano wote watajipatia kuwa chini ya utumwa kwa mtu yule.Kesi kama hizo zimechipuka,na wapendwa wametuandikia ili kupata mapendekezo kwa jinsi wanaweza kuwachana na ndugu kama huyo ambaye alikwisha kuwa kiongozi bila kumwudhi au kumwumiza.

Hiki kitendo cha kuchukua uongozi kimekuwa cha muhimu sana kwa vyovyote vile,na umechukuliwa kwa wale ambao wana nia njema sana,na wana matokeo mazuri hadi kiwango fulani,na kwa hivyo inafanyika wakati mwingine kwa wenye hekima.Ndugu aliyejawa na upendo wa ukweli na hamu ya kumjua Bwana anawasanya watu wachache kwake ambao wanapokea ukweli kwa furaha,ambao wana hamu na hitaji la kujua na kupata maagizo mengine zaidi,ambayo yeye,kama aliyepiga hatua,ana uwezo wa kupeana;na pamoja wanakua katika maarifa ya ukweli,na kwa juhudi ya pamoja kundi linaongezeka,hadi wanashauriwa kutoka kwa nyumba yao hadi kwa ukumbi wa kukutania.Kwa wakati huu,kina ndugu wengine wataonekana kuwa na uwezo wa kulinda kundi kubwa au kufanya kazi ya umma.lakini wote wanahofia kupendekeza kwamba ndugu mwingine aliye na uwezo achukue uongozi,kwa kuhofia kumkosea yule aliye na uwezo mchache hata hivyo anajulikana kwa muda mrefu na kupendwa.Kwa wakati mwingine,hata akipata kutambua jambo hilo dogo,anaweza kuwa na hisia ya chuki,na ni wazi kwamba ndugu huyo amekuwa na hisia kwamba yuko na nafasi kama mshika dau katika kundi hilo,na naongea na kuwataji kama watu wake,n.k.n.k sio kama Bwana wao.Lakini hiyo wakati mwingine siyo sababu,tunafurahia kwa sababu wakati mwingine tunaona neema na upole ukiendelea kukua,na ubinafsi unapotea kwa mtazamo wa kazi ya Bwana.

Pia wakati mwingine mtu ambaye amekosa neema ya unyeyekevu,na asiyezoea hali,anakuwa mtu wa mbele kwa kuchukua uongozi na ana hamu ya kuushikilia;na kama hajakomaa katika Imani,kundi hilo linaanza kukwaza na visio ama mafundisho ya uongo ambapo kwayo wengine wanaanza kuanguka.

(4) Ikiwa mipangilio ya utaratibu imekosekana katika Kanisa,wale ambao wanamtegemea katika maslahi yake,na wana hamu ya kuwa katika huduma yake,wanaweza kupatikana katika hali ya aibu sana.Uaminifu wa ukweli mara nyingi unaleta utengano.Na wengine ambao hawapendi uaminifu wanaweza kupinga kwamba huduma za walio waaminifu haitakikani,ila hiyo haiwezi kuwa kauli ya wote,hata siyo kauli ya watu wengi katika kundi.Mtu mwaminifu anaweza kukosa anayemwuunga mkono kwa kujieleza kamili,na anaweza kupigania kundi mtu mmoja na akishindwa atawaacha kundi peke yake,na kuwaachia katika neema ya adui.

Ukweli kwamba vitu vinaendelea kwa njia rahisi bila mpangilio  wowote uliokubaliwa,ama wajibu,haki na uhuru wa kusanyiko uliokusudiwa,siyo dhamana kwamba zitaendelea hivyo.Adui wetu aliye macho kila wakati atakuwa na nafasi mahali pasipozingirwa ama mahali ambapo hapana kanuni za Kanisa zilizowekwa pamoja,na hata kwa mtu binafsi wa kundi hilo.Kwa hivyo kama Kanisa,na pia kama mtu binafsi twaweza  "kutoacha mahali pasipolindwa,bila udhaifu wa roho lakini chukua kila fadhila,kila neema na kuimarisha zote."

Majira ya amani na kupumzika ni nyakati za kujiandaa kwa mambo ya dharura ya  dhoruba na tufani,ambayo sote kwa pamoja na kila mtu lazima apate.Huyo atakuwa nahodha asiyeona mbali na mfanyikazi ambaye ataweka chombo kwenye bahari ambacho kimetengenezwa kwa hali ya hewa iliyo ya wastani.Hekima inatushauri kwamba haijalishi kama hali ya hewa ni ya wastani,haijalishi kama bahari imetulia na  ganda la bahari linaleta kitulizo,mipangilio ya kukumbana na tufani lazima iwe-utoaji wa mashuaokozi,rungu ya kujilinda,ya kusgika miundu n.k.., lazima viwekwe tayari.Nyakati hizi za majaribu hasa wakati Shetani anafanya bidii na kuwa na ujuzi katika upinzani wake,twapaswa tuangalie silaha zote ambazo Bwana,kupitia kwa mitume,wametuhimiza tuwe nazo za kujilinda.

**SHAURI LA KIMITUME LIMEKUBALIWA.**

Kwa mtazamo ya mambo haya yanayotokea kwa dharura hatuna budi kukubali kwamba Makanisa katika sehemu yo yote,likiwa dogo ama kubwa,kwa shauri la wazee,kwamba kwa kila kutaniko,wazee wachaguliwe miongoni mwa idadi yao ili "kulisha" ama "kuangalia" kundi.Na kulingana na fundisho la Mtume ( ***1 Wakorintho 12:28,29***),kwamba Mungu ameweka wengine katika Kanisa wa masaidiano,waalimu,n.k,na wengine hawajahitimu sana,tunatarajia kwamba Bwana atatupatia wengine ambao watasaidia katika kila kutaniko,na twapaswa kuwatafuta ili tuwapate katika makutaniko kama vile Makanisa ya awali walivyofanya. Wakati wapendwa kutoka nje ya makutano wanaweza kusaidia kuanzisha kazi,na kwa kuwatembelea mara kwa mara wanaweza wakawachangamsha,  **kila kutaniko wanapaswa watayarishe wazee wao na kuendelea mbele na kazi ya Bwana wakati wanafunguliwa njia**. Uwanja wao wa kila

kutaniko ni maeneo yao,kulingana na vile wataendeleza ushawishi wao;na bidii ya utauwa na juhudi wanayo miongoni mwao haitakosa kuzaa matunda. Ikiwa ngano chache zinaweza kuwekwa ghalani,basi ushuhuda mkubwa wa ukweli unatatolewa.Injili hii ya Ufalme wa Mungu lazima ihubiriwe kama “ushuhuda”, na pia kwa kuwasanya “watu kwa jina lake.” Kusambaza vijitabu,kuwatembelea watu moja kwa moja,barua zinazotumwa kwa watu na kuwasiliana moja kwa moja ( kwa njia ya hekima na busara)-katika warsha na maduka,mitaani,na karibu na mahali pa kuotea moto-ikiongezwa na tabia ya Mkristo ya heshima isiyopunguka na huduma ya ukarimu kwa majirani,ni njia zote za busara katika msalahi ya ukweli,ambayo bidii haitapuuzia.Katika njia hizi mbalimbali wote wanaweza kuihubiri injili;kwa sababu wote waliotakaswa wameteuliwa kuhubiri injili,na hawahitaji mamlaka yo yote kufanya hivyo pasi na ile Bwana alitoa katika kuwateua kwa njia ya Roho Mtakatifu.Kwa ajili hiyo Bwana na Kiongozi aliteuliwa;na uteuzi huu unaendea washirika wote wa mwili wake,yaani Kanisa lake,-***Isa.61:1-3;Luka 4:16-21;1 Yohana 2:27***.

**FURSA YA KUCHAGUA WAZEE.**

---

Tunapendekeza kwamba katika suala la kuwachagua wazee nia ya Bwana inapaswa kuangaliwa kupitia wakala wa watu wake waliowekwa wakfu.Tuache Kanisa ( yaani wale waliopata wokovu katika damu ya gharama ya Mkombozi,na wamewekwa wakfu kwa njia kamili na yeye) watoe uamuzi wao wa mapenzi ya Bwana kwa kupiga kura;na hiyo ikifanywa mara kwa mara-tuseme kila mwaka-uhuru wa makusanyiko yatahifadhiwa,na wazee hawatapata aibu.Ikiwa bado inafaa,na mapenzi ya Bwana kuonekana,hakuna kizuizi kitakachozuia uchaguzi tena wa wazee hao hao mwaka baada ya mwaka bila msuguano wowote ama hisia mbaya kwa yeyote yule.

Kura ya Kanisa inapeana nafasi tu kwa kila mwumini mwenye haki na aliyewekwa wakfu kamili ili aonyeshe Imani kwa mapenzi ya Bwana katika suala-siyo mapenzi yake;kwa kuwa akiwa wa Bwana;anahesabu mapenzi yake kuwa yamekufa,na anagundua kwamba ni lazima atende na kuongea kama vile Bwana mwenyewe angeongea. Mbinu hii inawapa wote haki sawia na fadhila.Hii pengine ndiyo mbinu ambayo Tito na wengine walitumia walipokuwa wakiangalia suala katika Kanisa la awali;kwa sababu hatuwezi kufikiri kwamba walichagua wazee kiholela bila kushauriana na watu,ambao walikuwa wanafahamu kuliko wao,pengine wasiojulikana. Hii pia ndiyo mbinu ambayo imetajwa katika ***Matendo 6:3-5***.Kumbuka pia kwamba unachagua watumishi (wahudumu) na sio watawala au mabwana.Hii pia ni mbinu tofauti na mbinu zilizoko katika makanisa yaliyoenea kwa madhehebu tofauti,ambayo mengi wanazuia fadhila kwa kikundi cha “makleri” ambao wanaongoza watu kwa nguvu;na hata katika vile vitu ambavyo waumini wanapaswa kuwa na sauti.,suala hayako kwa mikono ya watu wa Mungu waliowekwa wakfu kamili,wana waliofunguliwa na kuongozwa na Roho ,walakini kwa mikono ya wasiowekwa wakfu kamili walio chini ya kifungo ya madhehebu,wakiheshimu mafundisho pamoja na utaratibu,sio theluthi moja ya wale ambao wanaweza kudai kwamba wamewekwa wakfu kamili kwa Mungu.Ili kwamba tuwe na hakika ni kwamba tuna nia ya Bwana tunapaswa kujua kwamba tumetambua katika kura pekee wale wanaokiri kuwa wamehesabiwa haki kupitia

Imani katika dhabihu iliyowakilisha (mbadala) wa Kristo,na kuwekwa wakfu kamili kwake.Ni vizuri kugundua basi kutambua mtu kama huyo kabla kura haijapigwa,kwa kuwauliza kuinua mikono yao au wakae kwenye viti ndani ya chumba kingine katika nyumba.Hii pia itasaidia wengine pia,kwa kujiweka wajulikane mbele ya nia ya wote kwamba Imani na uwekeaji wakfu unaleta ushindi ,na kutoa ushuhuda wa maungamo haya mazuri mara nyingi kunaleta mibaraka kwa wale waliowekwa wakfu.

Ukweli ni kwamba wachache wanaweza kuwa waaminifu na taaluma zao,lakini kura ya wengi itakuwa chini ya mwelekeo wa Bwana,na maonyesho ya mapenzi ya Bwana;na kwa Imani kamili,inapaswa izingatiwe sana.Lakini bado inahimizwa na wengine kwamba licha ya kuwa makini katika kupata kura ya Kanisa pekee,kura ya watu wengi wa Kanisa bado inaweza kuwa na kosa,bila kuonyesha nia ya Bwana;na suala la uchaguzi wa Mathiya na mitume kumi na mmoja kujaza nafasi ya Yuda unaweza kutajwa kama mfano wa kushindwa,pamoja na kwamba Bwana alipuuzia chaguo lao na baadaye akafanya lake kwa kuchagua Paulo.

Huu,hata hivyo,haukuwa uchaguzi wa Kanisa chini ya mwelekeo wa Roho Mtakatifu;kwa sababu ilifanyika kabla ya Pentekoste,Roho Mtakatifu hakuwa amekuja ( ***Yohana 7:39***),na wanafunzi hawakuwa wametambulika na Mungu kama Kanisa.Pia,hakuna mtume yeyote alichaguliwa kwa njia hiyo kama vile wazee wa makusanyiko tofauti,na hata hawengechaguliwa hivyo:Kanisa ambalo ni mwili wa Kristo,halikuwepo.Kichwa cha Kanisa ndiye alikuwa ametambulika,na bado hakuwa ametukuzwa.Wale thenashara wote walichaguliwa moja kwa moja na Bwana,na baadaye wakahitimu kwa huduma yao ya pekee kwa mwili mzima.Kuchagua kwa “wazee kila mahali” kulikoamrishwa na mitume ni tofauti sana na uchaguzi wa mitume kumi na wawili wa Bwana,ambao kwao,Kanisa halikuwa na sauti yoyote,na halingekuwa nayo.

Kulingana na idadi ya wazee wanaotakikana kuchaguliwa katika kila kusanyiko:hiyo inategemea idadi ya waumini katika kutaniko ambao wamehitimu kwa huduma.Ikiwa wawili au watatu wanaweza kufanya kazi,huduma ya kutaniko ambayo inabadilishana miongoni mwao itawatosha kugundua talanta ya kila mmoja,ambao inaweza kupanuliwa zaidi ya kiwango cha kundi hilo;na kutaniko pia katika njia hii watapata neema kupitia kwa talanta nyingi.Ama kuna uwezekano wa kuwa na mtu mmoja au wawili ambao wanaweza kupewa kama wakionekana wamehitimu sana.

Wakati wa kuwachagua wazee unapaswa kuwa wakati muhimu sana.Ni shughuli za Bwana,na inapaswa kufanywa kwa makini kana kwamba inafanywa mbele yake Bwana.Ndugu ambaye anawakilisha kama mwenye kiti wa Mkutano anapaswa kujaribu kuonyesha kuwa makini mbele ya wote.Ikiwa mtu ye yote katika kutaniko anataka kujua na kufanya mapenzi ya Mungu peke yake,na kuwa katika maelewano na uwekeaji wakfu wake,akionyesha anayoamini kuwa mapaenzi ya Bwana katika suala,basi katika nguvu ya ahadi, “ Wenye upole atawaongoza katika hukumu” (***Zab.25:9*)**, matokeo ya mashauriano yanapaswa kupokelewa na wote kama wazo la Bwana,yaani Roho wa Mungu kama amenena na kupitia watu wake waliotakaswa.Kawaida matokeo ya mashauriano hayo yatakuwa makubaliano ya wote kwa pamoja.

**SIFA ZA WAZEE WA KANISA**

---

Katika ***1 Tim.3:1-7*** Mtume anaeleza sifa za mzee au mwangalizi,na katika mstari wa 8 hadi wa 13 sifa za mzee msaidizi zinaelezwa.Mistari hii inapaswa kusomwa kabla ya kura kupigwa,na mzee wa wazee wa kufanya huduma kubwa anapaswa kuchaguliwa kwanza,alafu,ikiwa wasaidizi wanahitajika,wanafaa wachaguliwe baadaye.Miongoni mwa wasaidizi hawa wanahitajika pia kina dada;kuna huduma ambazo zinaweza kufanywa kwa njia bora na wanawake wasaidizi,kama vile ***Warumi 16:1***;na inaonekana vizuri kwamba katika Kanisa la awali kina dada wengi walifanya huduma.Aina ya kura inapaswa kuangazia sifa ambazo zimetajwa kulingana na uamuzi wa kila mapenzi ya Bwana.Tunanukuu, -

" mtu akitaka kazi ya askofu [huduma],atamani kazi njema.[Kila huduma tunaofanyia mwili wa Kristo ni huduma ya baraka.] Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumiwa,mume wa mke mmoja [si lazima awe mwanaume ambaye ameoa;kwa sababu Bwana na Mtume walipendekeza hali ya useja kama ikiwa inahitajika ( ***Mathayo 19:12;I Wakorintho 7:32,33***),lakini asiwe na zaidi ya mke mmoja,kitendo ambacho kilienea sana wakati huo kuliko wakati huu],mwenye kiasi na busara,mtu wa utaratibu,mkaribishaji,ajuaye kufundisha,sio mtu wa kuzoelea ulevi,si mpiga watu;bali awe mpole;si mtu wa kujadiliana,wala asiwe  mwenye kupenda fedha,mwenye kuisimamia nyumba yake vyema,ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu;( yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe,atalitunzaje Kanisa la Mungu?”

Dhana sio kwamba,kama vile inavyoonekana,kwamba hawa watumishi wa Kanisa wanatawala Kanisa,-kuliwekea sheria na kuweka chini ya mapenzi yake,-lakini kwa hayo,pamoja na upendo wote,wanapaswa kuongoza kanisa,akiangalia masilahi na masuala yake na kuwashauri na kusaidia kama msimamizi mwaminifu wa Mungu.( Tazama mkazo.) Bwana Yesu ndiye Bwana ambaye Kanisa linahitaji;na hakuna sinodi,au baraza,au makasisi au wazee wanaruhusiwa kuchukua nafasi ya Bwana wetu pekee na Kichwa cha Kanisa.Wapendwa katika Kanisa wanaweza kushauri na kutoa mawaidha;lakini wanapofanya hivyo wanapaswa kujitahidi kuongea kila mara,lakini siyo mawazo yao,lakini kulingana na mausia ya Mungu._ “  Kila mmoja kwa kadiri aliyoipokea karama,itumieni kwa kuhudumiana;kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu,mtu akihudumu,na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa  na Mungu;ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo.” ( ***1 Pet.4:10,11***).Shauri lao lapaswa kuwa na uzito na Kanisa pekee likitekelezwa na Neno na Roho wa Mungu,wakizingatia kanuni na amri za Mungu,lazima shauri hilo liwe  na fikira za makini kwa wote,katika roho ya upole.Na ikiwa katika majivuno ya moyo,mtu yeyote amedharau agizo hilo,kwa kutoheshimu ama kwa kuchukuwa wepesi mtu ambaye Mungu amechagua kwa kuangalia  kundi lake,basi upinzani huo utakuwa dhidi ya Bwana na njia yake.

Ni kwa sababu hii ndiyo maana Mtume anatushauri kwamba “mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu,shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua,na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo” (***Waeb.12:15***); kwa sababu neema ya Mungu,na huruma yake,katika kuonyesha mapenzi yake na kuweka wazi katika Neno lake,zinawajia Kanisa kupitia  chombo chake yaani mwanadamu.Na ikiwa mtu yeyote,kupitia kwa vita au kujitukuza au kutoka kwa nia fulani,anatafuta kuharibu ujasiri wa kundi la Bwana,na kupanda uchungu katika mioyo yao dhidi ya watumishi hao kama vile Bwana alivyowaweka kwa kuonyesha na kuulinda ukweli,basi

anazuia neema ya Mungu kwa waumini,na matokeo yatakuwa ni kuchafua wengi.Ye yote ambaye anafanya hivyo yuko mkononi mwa hukumu ya Bwana,na hata kama wamekuwa na cheo gani basi kazi yake itakuwa bure na wote wanaomfuata wataenda kwa njia kombo.Ikiwa wapendwa ambao wamekuwa waaminifu kwa Bwana wakitofautiana wenyewe na manufaa yao kutofautiana katika kuamua mapenzi ya Bwana,wanapaswa kutofautiana tu kwa upendo,na wanapaswa kujitahidi kwa maombi na kusoma kwa makini na kwa jitahada zaidi wajaribu kusafisha mioyo yao kutoka kwa tabia ambayo itawafanye wakose kustahili kwa ukweli,na waje haraka katika umoja wa imani-“ Basi sisi tulio wakamilifu [ katika mioyo,mapenzi],na tuweze hayo;na hata mkiwaza mengine katika jambo lo lote,Mungu atawafunulia hilo nalo.Lakini hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo.”-***Wafilipi 3:15,16***.

“Sio mtu anayejifunza [ asiye na uzoefu au asiyeweza kujaribiwa],pengine apate kushikwa na kiburi,na kuanguka kwa hukumu ya Shetani [k.v.kama vile Shetani-***Isa.14:13,14;Wafilipi 2:5-9*** *Diaglott*-alafu apate kujiona kuwa mtu mkuu ,na kuanza kuonyesha unyonge wake;kwa sababu kiburi kinaleta uharibifu na roho yenye maringo huanguka]”

" Tena imempasa kushuhudiwa mema [ kwa uaminifu na maadili mema] na watu walio nje ( wa ulimwengu);ili asianguke[katika unafiki] katika lawama na mtego wa Ibilisi."

"Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu,si wenye kauli mbili,si watu wa kutumia mvinyo sana,si watu wanaotamani fedha ya aibu,wakilishika siri ya imani katika dhamiri safi.Hawa pia na wajaribiwe kwanza;baadaye waitende kazi ya shemasi,wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia.Vivyo hivyo na wake zao na wawe wastahivu;si wasingiziaji;watu wa kiasi,waaminifu katika mambo yote.Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja,wakisimamia watoto wao vizuri,na nyumba zao."

Katika barua zake Tito Paulo anaongeza kwa sifa yafuatayo, “Mkishika Imani ya neno,kama vile ulivofundishwa ili kwamba kwa mafundisho,kwa kuhimiza na kushawishi wanaongea vibaya,kwa sababu kuna wengi walio na kiburi na wanaoongea maneno yasiyo na maana na wadanganyifu,..ambao midomo yao lazima ikomeshwe.” Ni jinsi gani ustawi wa kundi litaonekana kupitia kwa sifa za wazee waliochaguliwa! K wa vyovyote vile wanafaa wachague wale “walio na Imani dhabiti,” ukizingatia Neno la haki,” na kuepukana kwa makini wale ambao wanakabiliana katika ubashiri wa wanadamu na filisofia zisizofaa.Tahadhari hii pia inaonyesha kwamba Kanisa linapaswa lijue vizuri Imani yao,na kuweza kujua Imani ya wazee wao.Imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja ( “Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu”) lazima watathmini kila kipengele cha ukweli uliokomaa na kufuatana.Na visio vyote vya kubuniwa na filosofia ni mambo ambayo yanafaa yaachwe kama vile Mtume alivyosema.-***1 Tim 6:20***.

**WAJIBU WA KIMITUME KWA WAZEE.**

---

Basi wakati wazee wamechaguliwa na wamekubali huduma ,wajibu wa Paulo kwa Timotheo ***( 2 Tim.3:16,17;4:1-5***) na ***Tito 2:1,7,8,11-15***), na wa Petro katika barua yake ya kawaida ( ***1 Pet.5:1-11***),wanaweza kusomewa mbele ya kutaniko,ukifuatwa na maombi kwamba Mungu

ataongeza baraka yake juu ya wazee walioteuliwa,na juu ya kutaniko lote watakaoshirikiana katika huduma ya Bwana.

"Maneno hayo ya Mitume  yanavutia sana. Sikiliza Paulo: “Kila andiko ,lenye pumzi ya Mungu,lafaa kwa mafundisho,na kwa kuwaonya watu makosa yao,na kwa kuwaongoza,na kwa kuwaadibisha katika haki;ili mtu wa Mungu awe kamili,amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.”

"Nakuagiza[Timotheo] mbele ya Mungu,na mbele za Kristo Yesu,atakayewahukumu walio hai na waliokufa;kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake,lihubiri neno,uwe tayari,wakati ukufaao na wakati usiokufaa,karipia,kemea,na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.Maana utakuja wakati *watakapoyakataa mafundisho yenye uzima*,ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi,kwa kuwa wana masikio ya utafiti;nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli,na kugeukia hadithi za uongo,Bali wewe,uwe na kiasi katika mambo yote[dhidi ya ushawishi mabaya na mielekeo],vumilia mabaya [kwa sababu watawajia wote ambao ni waaminifu kwa huduma,wale watakaokumbana na ghadhabu ya adui ambaye atawapinga kwa nguvu],fanya kazi ya mhubiri wa Injili,timiliza huduma yako"

Kwa Tito anasema, “Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima….katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema,na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu,na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa,ili yule mwenye kupinga atahayarike,kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu…Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa;nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia;tupate kuishi kwa kiasi,na haki,na utauwa,katika ulimwengu huu wa sasa;tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu,..Nena maneno hayo,onya na kukaripia kwa mamlaka yote[mamlaka ya Neno la Mungu,siyo yake Tito];asikudharau mtu awaye yote.”

Sikiliza Petro pia: “Nawasihi wazee walio kwenu,mimi niliye mzee,mwenzi wao,na shahidi wa mateso ya Kristo,na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye;lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu,na kulisimamia,si kwa kulazimishwa[lakini kwa kuwahimiza],bali kwa hiari [kukubali kuchukua kazi na majukumu ya huduma] kama Mungu atakavyo,si kwa kutaka fedha ya aibu,bali kwa moyo[ambao unapenda kuhudumia Bwana,wanakondoo na ukweli] .Bali si kwa wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao,bali kwa kujifanya vielezo kwa lile kundi.Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa,mtapokea taji ya utukufu,ile isiyokauka.Vivyo hivyo ninyi vijana,watiini wazee.Naam,ninyi nyote jifungeni unyenyekevu,mpate kuhudumiana;kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi,lakini huwapa wanyenyekevu neema.”

“Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari,ili awekweze kwa wakati wake;huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote,kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.Mwe na kiasi na kukesha;kwa kuwa mshtaki wenu Ibilisi,kama simba angurumaye,huzunguka-zunguka,akitafuta mtu ammeze.Nanyi mpingeni huyo,mkiwa thabiti katika Imani…Na Mungu wa neema yote,aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo,mkiisha kuteswa kwa muda kidogo,yeye mwenyewe atawatengeneza,na kuwathibitisha,na kuwatia nguvu.Uweza una yeye hata milele na milele.Amina.”

**MAZOEZI YA UHURU YANATULINDA DHIDI YA UTUMWA**

___________

Wengine wamefurahi kwamba wako huru kutoka utumwa wa Babeli kiasi kwamba wanahitaji tahadhari dhidi ya kinyume kinachokithiri-yaani ukosefu wa mpangilio.Wengine wanaogopa utumwa wa madhahebu ya kidunia kiasi kwamba wanahofia kutumia uhuru wao kutambua idadi yao ambao wameamini wanaweza kuwa wamechaguliwa kwa huduma fulani ya Bwana.Kwa hivyo wanaingia kwa utumwa ambao wanapaswa kuepa.Tabia ya wote ni kama timazi iendeyo hadi mwisho sana,lakini mtindo wa Neno na roho wa ukweli ni “ kusimamisha,kuipa nguvu,na kuituliza.” Maslahi ya kiroho ya kundi la Bwana katika mahali popote ni masuala makubwa sana na muhimu ambayo si vizuri kuachwa kwa hali yasiyo mazuri ambayo Shetani ana uhakika na anaweza kupata nafasi kwayo kwa wakati mwingine.

Hakika kwamba tumeachana na utumwa wa Babeli,siyo sababu ya kuwacha mipangilio yote na mfumo katika masuala yetu:Kanisa la awali pengine walikuwa na hofu kama hiyo;kwa sababu walikuwa wametoka kwa utumwa wa Uyahudi,na waliagizwa wasishikwe tena na nira ya utumwa. ( ***Wagalatia 5:1***) Nira ya utumwa,hata hivyo haikuwa dhana ya mfumo na mpangilio.Lakini utumwa wa Imani ya kale ya Uyahudi-Agano la Sheria.Kutoka kwa hiyo wangebaki huru;kwa sababu Kristo,kupitia kwa dhabihu,amewafanya huru.Kwa dhahiri utaratibu wa mpangilio uliodhihirishwa kwa Makanisa na kutumiwa na wote haukuchukuliwa kama utumwa,mpangilio ulisimamishwa na wazee walioteuliwa katika kila mahali;na kazi ya Bwana kuendelea.kwa njia ifaayo.

Kanuni ya mpangilio na kuwatambua wazee walioteuliwa kwa njia ifaayo na waliohitimu kwa roho wa Bwana-sio kwa zinazoitwa chuo cha Biblia-na kuwadumisha katika kazi zao kwa kuidhinisha na ushirikiano wa kutaniko wanalohudumia unafaa,la sivyo Mitume walikosea kwa kuuagiza mpangilio huo kwa Kanisa la awali,na Wakristo wa awali pia walikosea kwa kutopinga mpangilio huo.Lakini hakika Mitume na Kanisa la awali hawakukosea.Mpangilio na utaratibu wa masuala yao yalithibitisha baraka,na Bwana mwenyewe alitengeneza historia katika kutambua mpangilio,wakati katika ufunuo wake kwa makanisa saba ya Asia,alitoa ujumbe wake kupitia kwa wazee wawakilishi, “malaika,” wajumbe na watumishi-***Ufu.2:1-8,12,18;3:1,7,14***.

Hatuna mabishano na makanisa wa kawaida katika mada ya utaratibu,lakini wamepita unyofu ulio katika Kristo,na utaratibu ambaye aliweka kupitia kwa mitume wake watakatifu,na wamezidisha aina za utauwa kwa kiasi kwamba wamepoteza nguvu zake.Hatuwezi kuupuzia kitu kwa sababu makanisa ya kawaida wamepuuzia,lakini twapaswa kukataa mabaya yote,chochote ambacho hakielewani na Neno na roho ya Mungu.Kama tungekuwa tunaoongozwa na uhasama wa madhehebu mengi,tungefikia ukingoni mwa kupuuzia ukweli wa ajabu ambao mifumo ya Wakristo bado wanashikilia kwa njia nyingine,japo sasa siyo kwa njia ya ushupavu.Tungepuuzia mafundisho ya upatanisho uwakilishi,au ya ubatizo au ya Pasaka,kwa sababu wameishikilia.Lakini kwa sababu tunafundishwa na Neno la Mungu,tumepata kushikilia lililo jema,na miongoni mwa vitu vizuri ni kufanya kila kitu kwa ajili ya Bwana,zaidi ya yote, “ kwa uzuri na utaratibu,” lakini uwe ni utaratibu wa Kimaandiko,lakini sio utaratibu wa Babeli,ambao

wanainua kikundi cha mabwana badala ya urithi wa Mungu na wanampuuzia Kichwa cha Kanisa,ambaye ndiye mamlaka ifaayo. Usisahau kwamba " Mmoja ni Bwana wenu,ambaye ni Kristo,na wote ni ndugu,lakini mtu akitaka kuwa mkubwa miongoni mwenu basi awe mtumishi." "Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu," na kwa mtazamo wa kuujenga mwili wa Kristo.-***1 Wakorintho 14:40,26.***

**HAKI ZA KICHWA YAANI KIONGOZI WA KANISA.**

---

Ni kosa kudhani kwamba Kanisa la kweli halina majukumu yaliyowekewa mipaka,kwamba tuko huru kufanya vile tunavyotaka,ama kwenda huku na kule kusanya mabakio ya vyakula kutoka kila meza,mbaya au mazuri na vinavyotofautiana.Ikiwa sisi tu wa Kristo,uhuru tu tunaofurahia ni uhuru wa kuwa mbali na utumwa wa dhambi na mauti na nira zote ambazo Shetani anaweza kutuwekea.Uhuru wetu umekuwa katika ukweli kwamba hakuna hukumu kwa wale walio kwa Kristo Yesu,tumetoka mautini hadi uzima,na sisi si watumwa wa dhambi.Mambo ya kale yaliyotutia utumwani yamepita,na mambo yote yamekuwa mapya.Huu ndio uhuru wa wana wa Mungu.Unagunduliwa kwa Imani na kwa kiasi sasa lakini hivi punde utagunduliwa zaidi wakati ambapo mwili huu unaokufa ( unaolaumiwa na una udhaifu kupitia kwa kuanguka) utavaa kutokufa.

Lakini tulipokombolewa na Kristo kutoka kwa utumwa wa Dhambi,basi tumefikia uhusiano wa agano naye ili tufanye mapenzi yake,ambayo pia ni mapenzi ya Baba wetu wa Mbinguni,kama vile Yesu alivyoaahidi na Mungu,akisema, " Sikuja kufanya mapenzi yangu,lakini kufanya mapenzi ya aliyenipeleka." Kwa hivyo,kama Bwana wetu aliyoeleza,sisi ambao alituweka huru kutoka kwa nira ya huzuni ya Shetani ametutwika nira na mzigo wa Christo-ambayo ni huduma ya furaha.(***Mathayo 11:29***).Huu basi ndiyo upana wa uhuru wetu ikiwa tu waaminifu kwa agano letu;na pia upana wa utumwa wetu.Jina lake lipate sifa! Twapat nira ya Bwana wetu na Mkombozi wetu mwepesi,na mzigo wake mwepesi,kwa sababu ya upendo wake kwetu na upendo wetu kwake.

Kanisa la Kweli la Mungu,"ambalo jina lake limeandikwa mbinguni," bila shaka ni shirika,hata kwa wakati huu,japo lina uwezekano wa kubadilika-yaani washirika wake wakipata kubadilika,n.k;lakini ni shirika la kibingu,si la kidunia.Kuna sababu mbili ambazo zinaweza kufanya Kanisa la kweli la Kristo linaweza kuzingatiwa: (1) Kutaniko lote la waumini toka mwanzo wa awamu ya Injili hadi mwisho linaunda mwili mmoja,Kanisa moja,siyo makanisa mengi,kwa sababu Bwana alisimamisha Kanisa moja.Na kwa Kanisa hilo moja,yeye mwenyewe ndiye "Bwana" na "Kichwa," "Mchungaji mkuu," na Mwalimu," na mamlaka pekee.Hili ndilo "Kanisa la wazaliwa wa kwanza," ambao "majina yao yameandikwa mbinguni" (***Waebrania 12:23***);na ambao majina yao yamezidi kuwa hapo hadi mwisho wa mwendo wao,na hawatatemwa kwa sababu ya kutokuwa waaminifu (***Ufunuo 3:5***),wataingizwa kama washirika kamili katika ushindi wa Kanisa wakati atatokea na ufalme wa Bwana na Mwokozi,Yesu Kristo.—***2 Tim. 4:8***; ***Tito 2:13***; ***1 Pet. 1:7; 5:4.***

Bwana mwenyewe anavitunza vitabu vya Kanisa-rekodi za majina yetu,na maelezo ya kila mtu,hatuna la kufanya kuhusu jambo hilo.Anasajili waumini wote waliowekwa wakfu,na hakuna nguvu zozote duniani zinazoweza kuwaondoa katika mkononi mwake,ama kuyatoa majina yao kutoka kwa rekodi zilizoko mbinguni.(***Yohana 10:28,29;Warumi 8:35-39;Ufu.3:5***).Hekima yake ya hakika pekee inatosha kwa hiyo,na kwa wote wa afisi ya Kichwa.Hata hivyo ni jambo lisilofaa na kukemewa kama mshirika wowote wa mwili wa Kristo akijifanya kuwa kichwa-akichukua mamlaka ya Kichwa cha Kanisa.Na mtu kama huyo asipokatizwa na kurekebishwa na Bwana,atakataliwa mbali na kuwachwa kama nje ya mwili wa huo wa Kristo.—***2 Wathes. 2:11***.

(2) Njia nyingine ambayo Kanisa linaweza kutambulika-ambayo pia ni njia ya Kimaandiko (***Filemoni 2;Ufunuo 2:1,n.k***.)-ni ya kuhesabu sehemu yake kama Kanisa zima.Kwa hiyo watakatifu wote wanaweza kuhesabiwa kama Kanisa la leo.Ama tena,idadi yoyote ya Kanisa hai lililokusanyika pamoja sehemu yoyote inaweza kuitwa Kanisa (K.v***. Filemoni 2;Ufu.1:4;2:1;2 Wakorintho 11:28***); kwa sababu mahali wawili au watatu wanakutanika,Bwana,ambaye ni Kichwa,ameahidi kuwa miongoni mwao.(***Mathayo 18:20***).Kusanyiko kubwa kutakuwa wakati washiriki wote wametukuzwa na kuunganishwa na Kichwa.

Ikiwa mtu atauliza kama twajua washiriki wa Kanisa la kweli,tunajibu,Tunawajua kwa kazi ya Imani katika Kristo,na kwa roho ya Kristo inayoonekana ndani yao.Ni ukweli wake,na roho yake,na uwepo wake unaonekana miongoni mwao,unawafanya wakusanyike pamoja,ambao unawauunganisha mioyo yao katika umoja wa upendo wa Wakristo na ushiriki,ambao unawatia msukumo na tumaini moja,unawahuisha na furaha,na kuwaongoza kushirikiana pamoja katika kazi ya Bwana.Ikiwa itaulizwa,Tunaweza fanyaje na yule ambaye aenendi kwa utaratibu miongoni mwetu kwa sababu hatuwezi kuondoa jina lake katika orodha ya washirika? Tunajibu,tunao mwelekeo ulio wazi katika hoja hii.Basi,kama vile katika Kanisa la awali,kuna viwango tofauti ya maendeleo miongoni mwa washirika,na Paulo anasema (***I Wathes.5:14***),wengine hawajakomaa,wafariji;wengine ni wadhaifu,wasaidie;lakini mkiwa na saburi kwa wote,waonye wasiokuwa wataratibu.Lakini baada ya kumwonya mtu kama yule kwa uaminifu,ikiwa bado hajatii ukweli, "mtazame mtu kama huyo ,na usiwe na ushirika naye ili apate kuaibika.Japo usimhesabu kama adui,lakini mhimize kama ndugu." Hadi ipate kuonekana kwamba Bwana amemtoa nje ili tusihisi udugu kwake.

Bwana pia anatoa mwelekeo katika masuala magumu ambayo yanachipuka katikati ya waumini.—***Mathayo. 18:15,17***.

Kichwa kikuu cha Kanisa pia ametoa njia nyingi ya kurekebisha watu wake-kwa kuwaajenga Imani iliyo takatifu sana na wa maendeleo yao katika tabia ya Ukristo.Basi tuna uangalizi wake ulio imara na unaongoza kote katika safari yetu ya kidunia.Yeye ndiye Kichwa,sisi tu mwili;yeye ndiye Mchungaji,sisi ni wanakondoo;yeye ndiye Jemedari,sisi ni wanajeshi.Basi tuko Kanisani kwa muda wa majaribio,kwa majaribu;basi sisi ndio wanajeshi wa Kanisa,katikati ya maadui,tukitumaini kwamba punde si punde tutaidhinishwa kama wanajeshi waaminifu na wanaostahili kuingizwa katika ushirika kamili katika Kanisa ambalo limeshinda,katika nguvu na utukufu mkuu.

Kwa hivyo tunaona vile Kanisa la Mungu limepangwa kabisa,chini ya Kristo,ambaye ni Kichwa,hata katika hali hii ya majaribio,tukisafiri katika nyika kuelekea nchi ya ahadi ya Kanani.Sote tuko chini ya amri za Amri Jeshi mkuu ambaye wote lazima wamtii na kumfuata ambaye atafikia wengine ambao wamebaki kwa watu wa Mungu.Ah,hapana,hatuko peke yetu,na hatuna uhuru kufanya mapenzi yetu kwa njia yoyote.Kila mtu yuko chini ya mapenzi ya Mungu katika Kristo,hata mawazo yetu na ushirika wetu katika Kanisa unategemea uaminifu wetu katika kugundua jambo hili na kuwa na utiifu unaochangamsha na wa upendo.Hatuwezi kufanya tupendavyo kwa njia yoyote:tuko chini ya sheria kwa Kristo,ambaye roho mtakatifu wake lazima atawale matendo na neno na mawazo yetu;na bidii yetu isiyopunguka lazima ilete kila nguvu yetu na karama yetu chini ya mamlaka yake.

Katika utumwa huu uliobarikiwa kwa Kristo,utumwa wa upendo,kuna dhana kuu ya uhuru,kama vile moja baada ya nyingine,pingu ya dhambi inaanguka kutoka kwetu.Ulimwengu na dhana zake na tamaa ya kuwania makuu iliyobatili,na ujinga,na kiburi,na ushirikina na woga zinakomaa kutuweka pingu tena,na madirisha ya mawazo yetu na mioyo yetu yanafunguka zaidi kwa upana kiasi kwamba nuru ya utukufu wa neema takatifu iweze kutiririka ndani,na mioyo yetu inafurahia na kuimba.

## TARATIBU YA KIMITUME TARATIBU YA BWANA

---

Kwa hiyo Kichwa kikuu cha Kanisa ametupangia mwendo wetu.Alisema, “Hii ndiyo njia,ifuate.” Ametuelezea masharti yote na mipangilio,n.k. na ni wajibu wetu kuyafuata maelekezo yake.Ni kwake ndiyo Mtume Paulo anaeleza mipangilio ya utaratibu wa masuala ya Kanisa,akisema:—

"Naye alitoa wengine kuwa mitume,na wengine kuwa manabii;na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu,hata kazi ya huduma itendeke,hata mwili wa Kristo ujengwe." (***Waefeso. 4:11-16***) Hapa, kama vile katika ***1 Wakor. 12:12-20*** Mtume anaeleza uhusiano wa Kanisa kwa kila mmoja na Bwana na sehemu ya mwili wa mwanadamu: na anasema kwa undani kwamba kila mshirika anapaswa kulishwa na kufanyiwa mazoezi,ili mwili uwe sawa,na timilifu.Na tena,mtume huyo anatueleza, “Mungu ameweka kila mtu,kila mmoja wao,katika mwili,kama alivyopenda.[Kila mtu anapaswa kutafuta na kugundua uteuzi wa Bwana kwake yeye mwenyewe,na pia kwa wengine,na kila mtu anapaswa kujitahidi kuhudumu kulingana na mpangilio wa Bwana unaotambulika pekee.]…Kwa sababu mwili sio mmoja lakini wengi… “Na Mungu amechagua katika Kanisa,wa kwanza mitume,wa pili manabii na wa tatu waalimu,n.k…,n.k.” Tunaamini kwamba Bwana amefanya jukumu lake,kila wakati katika awamu akitoa watumishi wake katika Kanisa;lakini watu wake hawajaangalia kuhitimu kwake na kuteuliwa kwakwe,na kwa hivyo wamekosea sana kwa kosa hilo,na kwa kukubali viongozi wa dini wanaojiteua,na kujiinua,na wanajiongoza na kujiendeleza.

Kulikuwako na mitume kumi na wawili,na huduma yao iliyotiwa msukumo ilikuwa ya Kanisa zima,mpaka mwisho wa dahari.Hawakuwa na waandamizi lakini Bwana mwenyewe alikuwa

akichagua waalimu na wachungaji waliokuwa na viwango tofauti vya uwezo kila wakati ambao wangeweza kuwaagiza na kulinda maslahi ya kundi.

Neno "mzee" laonekana kwamba linatumika kwa watumishi wote ambao Bwana amechagua katika Kanisa lake kwa kujenga maadili,wengine wao wakiwa na kazi kubwa wakati wengine wasaidizi.Kwa hiyo Mitume walijiweka kama wazee,( ***1 Pet.5:1)*** Neno "mzee" lingemaanisha kaka mkubwa,sio lazima awe na miaka mingi,lakini amekomaa katika tabia ya Kikristo.Timotheo na hata Tito walikuwa wachanga—***1 Tim. 4:11,12***; ***Tito 1:4; 2:15***.

Ikiwa kutaniko moja au mengi limeonekana kuwa na karama ya uwasilishaji wa hadhara ya ukweli,uwezo huo unafaa kutambuliwa na wote,na wote wanafaa washiriki kwa kutumia hiyo karama;na mikutano ya kipekee inapaswa kuandaliwa kwa ajili ya hiyo.Mikutano hiyo inaonekana kwamba haikuwepo katika Kanisa la awali,na wanenaji waliobobea kama Paulo ,Apolo na Petro hawakuwepo.Lakini,karama kama hizo zingepatikana,zingetumika na zilikuwa za manufaa ya huduma.Kwa hivyo zinafaa ziwe miongoni mwetu.Karama ya kuongea kwa umma inaweza kuwa ya kawaida au isiyo ya kawaida,lakini ilikuwa ya kujenga kwa njia yoyote ile.Mikusanyiko inapaswa kutathmini hiyo;lakini kama talanta hiyo haitapatikana basi hakuna haja ya mahubiri ya hadhara,lakini huduma nyingine ambayo yawezayo kujenga sana,na ile ambayo talanta nyingine za kufaa zaweza kupatikana katika kutaniko.

**MAMBO YA KUTAFUTA KATIKA MAKUSANYIKO YA WATAKATIFU**

Tazama pia mambo ya kutafutwa katika makusanyiko ya watakatifu na huduma ya wazee,n.k.Halikuwa starehe za kijamii,ama kuenenda kwa ratiba ya kawaida ya mfumo wa huduma,lakini ilikuwa (1) " kwa kukamilisha watakatifu wapate kufanya huduma."Haya makusanyiko yalipaswa kuwa shule za kufundisha,ambazo watakatifu wote wangeandaliwa ya kutosha kwa kazi [ "huduma"] ya Bwana-siyo tu kazi takatifu ya siku za usoni,lakini pia kazi muhimu inayotakikana ya Kanisa katika awamu hii ya sasa,ambayo bibi harusi "anajitayarisha" kwa kazi ya siku za usoni.Kwa wakati huu watakatifu wote wanafaa wawe wanafunzi wanaojitahidi,na maagizo yanafaa yawe ya utaratibu na ya mpango kama inavyotakikana,na pia kwa mtazamo wa bidii na maendeleo,pasi na maburudiko.Kumbuka kwamba Paulo alikemea wengine ambao hawakuwa wameendelea na kusimama kwa fursa zao,akisema, "Kwa maana,iwapasayo kuwa waalimu(wakati mwingine umepita),mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya neno la Mungu [mafundisho ya Kristo];nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu."—***Waeb. 5:12***.

(2) Ilikuwa ni ya kuujenga mwili wa Kristo,-kwa kuungana pamoja katika umoja wa imani na wa roho katika upendo na kujitoa kwa Mungu,ili kwamba kama mwili moja wanaweza kuendelea katika maendeleo ya tabia ya Kikristo na neema na maarifa kwa kimo cha ukamilifu wa Kristo.

Katika mtazamo wa jambo la kusanyika kwetu pamoja twaona kwamba tunayo kazi muhimu ya kutimiza.Kwa hivyo tusome tujionyeshe kuwa tumekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari,ukitumia kwa halali Neno la kweli.Pia katika mtazamo huu wa mada

ambayo tumekuwa nayo tumependekeza mpango unaoitwa “Mzunguko wa Mapambazuko ya Kusoma Biblia” uliotajwa katika makala ya Septemba 15,na kama kifaa cha bidii nyingi na mfumo wa kujitayarisha kwetu kwa utumishi,na kama njia mojawapo ya neema;bali siyo peke yake.

Tunashauri kwamba mkutano mmoja uandaliwe kila wiki kwa kusudi hilo,kwa siku ya Bwana,au jioni ya siku moja katikati ya wiki.Ikiwa tumeamini kwamba mpango wa zama ndio mpango mtakatifu,chakula katika majira haya ya mavuno,na kwamba ni nyakati na majira ya uteuzi takatifu,basi dhamana ya kutia bidii katika kusoma ,ili kwamba tuwe na uwezo wa kutoa sababu ya Imani iliyo ndani yetu,haiwezi kupuuziliwa.Ndiyo tunayoitaji ili kujilinda kwa migogoro ya “siku ya uovu”-yaani nyakati hizi “mbaya,” na kwa kusudi hili ambalo bila shaka tulipewa na Mungu.Katika mikutano kama hii walio na nguvu wanaweza kuwa wa manufaa kwa walio dhaifu wakiwasaidia kuvaa silaha zote za Mungu na kwa kuonyesha jinsi ya kila andiko linaloletwa linaingiliana na mafanikio ya kutosha katika mpango mtakatifu,ambao ni mmoja wa ajabu na wakuridhisha kwa jumla.Hii na mikutano yote inapaswa kila wakati kutangulizwa na kufungwa na nyimbo za sifa na kuabudu.

Tunapendekeza pia mkutano wa katikati ya wiki ((wa kujitoa na iliyo na tabia ya kushirikiana,siyo ya kimafundisho),ulio na maombi,sifa na ushuhuda;sababu ya kufanya hivyo ni kuleta roho ya kujitoa na ushirika wa Kikristo,upendo na umoja.Kwa hiyo tunaweza kuhimizana na kuamshana kwa kufanya kazi njema.Kipengele muhimu katika mikutano hii yote ni fursa zinazotolewa kwa wote ili wapate kushiriki kwa uhuru na kupata kujijenga.

**UTARATIBU ULIOKO KATIKA KANISA LA ALLEGHENY.**

---

Ni jambo la muhimu sana na faida kwa watu wengi kujua utaratibu wa Kanisa hapa Allegheny.Ndiyo,hatuna orodha ya ushirika kwa sababu twaachia Mungu jambo la kutunza idadi.Yuajua wote walio wake;na tunawatambua kwa Roho yake aliye ndani yao.Tunakuwa na mahubiri,maombi na sifa katika lugha ya Kijerumani kutoka 7:30 hadi saa 8.30 jioni,na katika Kiingereza ni saa 9 jioni kila siku  ya Bwana,na Somo la Biblia ya kawaida kwa wote wakati wa jioni kuanzia saa 7:30 na ikifuatwa na sifa ya muda wa nusu saa ya huduma ya sifa.

Kama vile tumetawanyika kiasi cha kwamba hatuwezi kukutana katikati ya wiki,tumekuwa na mikutano ya nyumba kwa nyumba,katika sehemu tofauti tofauti ya miji hii miwili,siku ya Jumatano jioni;na masomo ya “mzunguko wa Mapambazuko unaanza Ijumaa jioni.Baadhi ya kina ndugu walio na uwezo wamechaguliwa kwa kura ya washirika ili  mikutano,na kwa mwisho wa kila kipindi wanabadilishana ili watoe mafundisho tofauti kwa makutaniko,na ni vyema kuwafahamisha viongozi na masharti ya kiroho ya kanisa zima la mahali hapa,Wachache pia wakati mwingine wanaenda kwa miji ya karibu kuwasaidia vikundi vidogo.Juhudi yetu ni kusaidia na kuendeleza talanta nyingi inwezekanavyo katika Kanisa,wakati mwingine jina moja au jingine linatolewa kutoka kwa orodha katik mwisho wa kipindi na majina mapya

yanapeanwa,na baada ya muda majina yale yanaweza kutumika na kupigiwa kura katika huduma.

Pamoja na viongozi waliochaguliwa na kutaniko kuna idadi ya kina dada ( kumi kwa idadi ya wote),ambao wanashirikiana na kina ndugu katika huduma ya jumla ya uchungaji.Hawa kina dada wanachaguliwa kwa kuangalia uwezo wao na nafasi walio nayo,n.k.kwa kufanya huduma.Kazi yao ni ya kuhudumia kina dada wenzao,wakati kina ndugu ambao wanaongoza mikutano ya jioni wanaangalia hasa kina ndugu wenzao.

Hii haizuii wajibu na haki ya wote katika kuwahudumia kila mmoja,lakini inahakikisha huduma kwa wote kwa njia ya taratibu,ambao kwa wakati mwingine unaweza kupuziliwa,kwa sababu wote hawaishi pamoja ili wawe na wakati unaotakikana,n.k.,kwa amri zao na pia wakati wetu umeshikiliwa kwa njia tofauti bado unafanya kushiriki katika huduma hizi za uchungaji kuwa bila usaidizi.

Mwisho wa kila kipindi tunakutana pamoja na kina ndugu na dada wanaosimamia kundi na kushauriana kuhusu hali za kiroho na mahitaji ya Kanisa la hapa.Tunafurahi kusema pia,kwamba hatujawahi kuona ugomvi au udhihirisho wa fitina au kujipendekeza miongoni mwa watumishi.Kazi inafanywa na kukamilishwa katika roho ya upendo na upole,na hamu ya kutenda wema,na inabarikiwa zaidi kwa kulijenga kundi la watu walioko hapa.

**UHUSIANO WA MAKUSANYIKO NA WAZEE.**

---

"Bali ninyi msiitwe Rabi [mtu mkuu,mwalimu];maana mwalimu wenu ni mmoja,nanyi nyote ni ndugu;" na kwa kusanyiko ya watu wake pia anasema, "Wala msimwite mtu baba duniani;maana Baba yenu ni mmoja,aliye wa mbinguni.Wala msiitwe viongozi[ama checheo chochote msiitwe];maana kiongozi wenu ni mmoja,naye ndiye Kristo."—***Mathayo. 23:9,10***.

Hakuna alama ama tepe ya kutofautisha au makaribisho ya heshima yoyote hairuhusiwi katika mwili wa Kristo.Hakuna ndugu ye yote,hata kama ni ya manufaa au muhimu,anapaswa kuwa na hamu ya kupokea kutoka kanisa bila malalamiko au kukemewa; na mtu ye yote asisahau himizo la Bwana kama vile alivyonena. Ninyi nyote ni ndugu-ndugu walio na nia ,moja na sisi sote tuko chini ya udhaifu;na kila mtu ajue kwamba "hakuna mtu ye yote anaweza kuwa kizuizi [ kwa kiburi au ubatili au chochote kile kibaya],au kwa njia yoyote ya kuanguka,katika njia ya ndugu yake." Wengi kwa ukweli wamekuwa watu mashuhuri katika Kanisa ambao wameingiliwa na kujipendekeza –kujisifu kuikofaa,heshima ya kuabudu binadamu-ambayo inachipuka kutoka kwa dhana usiofaa kwa kikundi ambayo kina ndugu wanaowahudumia katika mambo ya kiroho wamewekewa majaribu au uwezekano wa kujikwaa. Ni kukosa kutii amri ya Bwana ndiyo inaleta nafasi ya ndugu anayeongoza kupata kicho cha pekee.Ni kujipendekeza kwa wazee wa Matengenezo Makubwa ambako kilidumu katika harakati ya kazi nzuri na ikaleta wengi wao waliokuwa na kuelewa kupoteza msimamo waliokuwa nao. (***Dan. 11:34,35***) Lakini halifai jambo hilo liwe miongoni mwetu:wacha kila mtu ajaribu kuzuia mwenziwe kutoka kwa majaribu na

kutengeneza na kujijenga katika kila kanuni ya haki na ukweli,na kwa kiasi ya mawazo na kuwa makini dhidi ya ushawishi wote wa roho ya ulimwengu inayolewesha.

Hata hivyo,kuna tofauti kubwa kati ya upendo mkunjufu na huruma na shukrani ya huduma ya uaminifu,na fikra isiyokamilika ambayo ina harufu ya roho ya ulimwengu,na kila mara ni kigeugeu kwa sababu ni ya uongo.Mkristo wa kweli mara nyingi atakataa kila kitu ambacho kinaleta harufu ya heshima ya kuabudiwa na kujipendekeza na akipewa majina hayo ya heshima ya kidunia,atasema,katika matendo au kwa maneno, "usifanye hivi;mimi ni mjoli wako…Msujudie Mungu" (***Ufunuo 22:9***);lakini wale ambao hawajakomaa watafurahia na kupokea maneno hayo kwa majeraha yao.Hii ndiyo maana Mitume wanashauri kwamba uchaguzi wa mzee viongozi uwe kwa wale waliokomaa kitabia,badala ya "mgeni." Wakati Bwana alipanga kwamba Kanisa linapaswa kuwa na viongozi ambao wengine ni mitume,wengine wazee,wengine wachungaji,wainjilisti,n.k,hangetuacha tutumie jina lolote kama cheo cha sifa;kwa hivyo,wakati tunatambua nafasi za huduma katika Kanisa,twapaswa kuwaita hawa viongozi-ndugu wapendwa katika Bwana.

Wakati Kanisa linalindwa kwa njia nyingine dhidi ya roho ya kidunia ya utukufu wa binadamu,linalindwa pia dhidi ya mwelekeo wa ubaridi,kukosa shukrani ambayo katika wivu,roho ya ufarisayo inasema kwa wazi, "Mtukuze Bwana,twajua kwamba huyu mtu ni mfanya dhambi." "Lakini ndugu,tunataka mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu,na kuwasimamia ninyi katika Bwana,na kuwaonyeni;mkawastahi sana katika upendo,kwa ajili ya kazi zao—***1 Wathes. 5:12,13***.

Pia anasema, "Watiini wenye kuwaongoza,na kuwanyenyekea;maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu,kama watu watakaotoa hesabu,ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua;maana isingewafaa ninyi.-***Waeb.13:17***.

Kwa hiyo,wakati wazee wanaonywa dhidi ya kujifanya kuwa mabwana juu ya urithi wa Mungu urithi,kundi pia linaonywa wasipuuze wazee,lakini siyo kuwafuata bila kuwajua na kuawaabudu bila kuthibitisha mafundisho yao kwa Neno la Mungu,,lakini kwa yote,katika unyenyekevu na upole,tushirikiane pamoja nao kwa Imani kama mwili mmoja kwa ajili ya kuujenga mwili mwenyewe katika upendo na katika neema ya Ukristo,na kwa kuendelea kwa jumla ya kazi ya Bwana.—***1 Pet. 5:1-11***.

**UMOJA WA MWILI WA KRISTO**

———————

Kabla hatujaacha mada hii ya kipekee ya utaratibu katika Kanisa,twapaswa pia kuangalia kwa makini muundo wa Bwana kwamba Kanisa zima (hai),japo limetwanyika ulimwenguni kote,linapaswa kushikamana pamoja.Ilikuwa hivyo katika siku za Mitume,na inapaswa kuwa hivyo hata leo.Ni kwa ulekevu mzuri kwamba,hata kwa njia ngumu ya kuwasiliana,wakati nafasi ilipopatikana katika makanisa sehemu moja ilibidi kuituma salamu na shukrani kwa wale walioko sehemu nyingine. (***Matendo 15:23***; ***1 Wakor. 16:19***; ***2 Wakor. 13:13***; ***Wafilipi. 4:21-23***; ***Wakolosai. 4:14,15***; ***1 Pet. 5:13***; ***Tito 3:15; 3 Yohana 14***); na wote walikuwa chini ya sheria

iliyowekwa na mitume,wakiwa na “Bwana mmoja,Imani mmoja,na batiso moja.” Juhudi yao ilikuwa ni kutunza “umoja wa imani katika dhamana ya amani,” na kuepukana mgawanyiko katika mwili wa Kristo.—***Waefeso. 4:3-13***; ***1 Wakorintho. 12:25***.

Kulionekana pia umoja mwafaka wa roho na Imani,na ushirikiano ulio imara,uliokuwa miongoni mwa mitume na wazee wa Kanisa la awali.Wote walikuwa na juhudi yao ya kuhubiri “ kitu kimoja,” yaani “mafundisho” ya ukweli ambao walipata kushawishika.Hakuna mtu alifanya bidii kupumbaza mwingine kwa kupata nadharia mpya iliyo yake mwenyewe.Apolo hakufanya bidii kupuuzia mafundisho ya Paulo;na hata wazee wa makutaniko madogo hawakufanya bidii ya kuwaongoza wanakondoo walio chini yao kwenye njia ya ubashiri na filosofia isiyo na maana.Hapana,hawakufanya hivyo,hata hivyo kila wakati waalimu wa uongo walikuja miongoni mwao na roho chafu ya kujitukuza wakijarinu mambo haya,wakitaka kupata wanafunzi wawafuate;lakini wanafunzi walio wa kweli,kwa upande mwingine,walikuwa waaminifu kwa kila mmoja,kama vile walivyokuwa kwa Bwana.Paulo alipanda,Apolo akatia maji,bali mwenye kukuza ni Mungu.

Tunafurahi kusema kwamba kwa sehemu kubwa roho hii inaendelea leo hii,na tunatumai kwamba itazidi kuendelea na kushinda,hadi tutakapofika katika umoja wa Imani kwa kufika kwenye cheo cha utimilifu wa Kristo,kama mwili mmoja chini ya Kichwa,Kristo Yesu,kwa amani kwa kushirikiana pamoja katika kufanya mapenzi yake kwa mwelekeo wa neno lake,tukifungamana katika upendo na jitihada katika huduma ya Bwana-yaani kazi kuu ya mavuno.

## SHIRIKA LA KANISA LA KIBINGU NA LA KIDUNIA

Tukiendelea tumeona uzuri,unyofu na ukamilifu wa shirika la Kanisa ambalo majina yao “yameandikwa mbinguni.” Mtawala wake na Kichwa ,Bwana Yesu,hana dosari;Mungu amemwekea mamlaka katika mikono yake,na kila mshirika wake anatakikana kutoa utiifu wa upendo,kifalme na wa upesi kwake,siyo kwa maneno na tabia tu bali hata kwa kila mawazo yao.Yeye ndiye anajua washirika na ikiwezekana anawatoa wale wasio waaminifu,na “kuyaondoa” majina yao.

Washirika wake,wakiungana pamoja kwa Kichwa chake,na pia kwa kila mmoja,kulingana na kiwango cha kukua kwao katika roho ya upendo wa Bwana wao,wanatakikana kutambua kama “ndugu” wote wanao roho ya upendo na kuwekwa wakfu na “Imani iliokabidhiwa watakatifu” – kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kulingana na Maandiko,na kwamba ameishi akituombea.Wanatakikana kukutana pamoja na kujijenga na kufanya mkutano yao na taadhima na utaratibu na kuwaangalia miongoni mwao kama vile Neno la Bwana na maongozo yanaonekana kuwekwa na kuwangalia wazee wanaostahili na kuwapa utambuzi wa umma (kama kwa njia ya kura kwa mfano) na kuwaruhusu kufanya huduma.Kanisa hili haliitaji kupangwa kwa sababu limepangwa tangia Pentekoste;na ikiwa mkutano mpya umeanzihwa ni muhimu kutambua ushirika na Kichwa na sheria zake,na kuzitii.

Basi kuna tofauti kubwa kati ya utaratibu huu na kanisa la kidunia,ambalo limepangwa kulingana na mapokeo ya wanadamu! Pamoja na makasisi wanaojiteua ambao ni mabwana juu ya watu wa kawaida huku wakigawa miongoni mwao marupurupu wanaochukuwa kutoka kwa watu wao- faida chafu,utukufu,heshima,vyeo n.k.,-kutoka kwa papa wanaofanya kwamba hawana dosari hadi "kwa wahudumu walio kwenye ngazi ya chini," ila wachache wamekuwa wahudumu wa kweli (watumishi wa kundi la Mungu);wengi wao wanajifanya mabwana juu ya urithi wa Mungu kwa kiasi ambacho waumini wao wanaruhusu.Soma kwa makini ***Yeremia. 23:1-4***; ***Ezekieli. 34:1-16***.

Mshikamano wa upendo katika Kanisa la kibingu ni shirika la kidunia ambalo limechukuwa nafasi ya mshikamano wa kibinafsi ya kiburi cha madhehebu na hofu kwamba ukifa nje ya kanisa la kidunia italeta adhabu ya milele.Kwa maungamo mepesi lakini ya nguvu ya Imani katika Kanisa la kibingu,wanabadilisha na kuleta migawanyiko-wakifanya maungamo na majaribio.Kwa ukweli nguvu za makanisa ya kidunia iko ndani ya tamaa za kimwili na kutojua Neno la Bwana kwa wafuasi wao na uhuru wao wa kibinafsi.Imani yao ya kibinafsi,maoni na uhuru wa washiriki wao wanajisalimisha kwa kusanyiko wakati wanajifunga na majina ya madhehebu,wajibu na maungamo ya Imani;na maono na uhuru wa kusanyiko baadaye inawachwa kwa wazee wa kanisa wanaotawala na makongamano,au kwa papa wa kidunia.Katika shirika la kibingu mtu ye yote anaweza kutoa ushauri na kutoa Neno la Bwana;lakini hakuna mtu ye yote awezaye kukiuka sheria na kukosa kuwekwa nje na Kichwa kikuu cha Kanisa asiye na dosari.

Uhuru wa kila mmoja wa washirika wa Kanisa la Kibingu kwa mshirika mwingine,na unyenyekevu wa kila mmoja kwa Bwana pekee ni tabia ya shirika la Bwana ambayo inatofautiana na mashirika ya wanadamu.

====================